

**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA  
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI,  
MHESHIMIWA AL HAJJ DK. ALI MOHAMED SHEIN,  
KATIKA BARAZA LA IDD EL FITR  
JUNI, 2018 (1 SHAWWAL,1439)**

**BISMILLAHİ RAHMANI RAHİM**

**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan;  
Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi;  
Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman;  
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa  
Umma na Utawala Bora,**

**Mheshimiwa Sheikh Saleh Omar Kabi;  
Mufti wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume,  
Rais Mstaafu wa Zanzibar;**

**Mheshimiwa Dk. Mohamed Gharib Bilal;  
Makamo wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania,**

**Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid;  
Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar,**

**Mheshimiwa Omar Othman Makungu;  
Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Sheikh Khamis Haji Khamis;  
Kadhi Mkuu wa Zanzibar.**

**Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri;  
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,**

**Dk. Abdulhamid Yahya Mzee  
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi,**

**Waheshimiwa Mabalazi,**

**Viongozi mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,**

**Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

**Wageni Waalikwa,**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana,**

**Assalam Aleikum Warahmatullahi Wabarakatuh**

### **IDDI MUBARAK**

Kila sifa njema anastahiki Allah Subhaanahu Wa Taala, Aliyetupa uhai, afya njema na uwezo wa kuitekeleza na kuikamilisha ibada ya saumu kwa salama na amani. Kwa uwezo na rehma zake, Mola wetu Mtukufu, leo tumekutana hapa ikiwa ni siku ya furaha kwetu kwa lengo la kutoa shukrani zetu kwake na kujipongeza kwa kutekeleza amri yake aliyotupa ya kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **Alhamdulillah!**

Sala zetu na salamu tunaomba zimshukie Mtukufu wa daraja, Mtume wetu Muhammad (S.A.W) pamoja na Aali zake, Sahaba zake na Wafuasi wake wote waliofuata njia yake ya haki. Mwenyezi Mungu atujaalie sote tuwe miongoni mwao.

Baada ya kumsalia Mtume Muhammad (S.A.W), nawaombea rehema na maghfira wazee, ndugu, jamaa, wahisani na Waislamu wote waliokwishatangulia mbele ya haki. Allah awajaalie makaburi yao yawe nyumba katika nyumba za peponi kwa baraka za siku hii ya Idd el Fitr. Tunamuomba Mola wetu Mlezi azikubali saumu zetu na ibada nyengine zote tulizozifanya katika Mwezi huu Mtukufu na miezi ijayo. Allah atuzidishie imani, uwezo na tuyafuate aliyotuamrisha na kuyaacha yote aliyotukataza.

### **Ndugu Wananchi,**

Natoa salamu zangu za dhati za Iddi kwenu nyote mliohudhuria katika Baraza hili na kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba. Kwa hakika, kuitekeleza na kuikamilisha kwetu ibada ya saumu katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni sawa na tulioshiriki katika mafunzo ya kina ya kupigwa msasa. Mafunzo hayo yametuzindua katika uchamungu na yametuzidishia imani ya kumuweka mbele Mwenyezi Mungu kwa kila tunalolifanya katika maisha yetu. Waumini wengi walizidisha kasi katika kusaidiana, kuhurumiana na kuvumiliana. Katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tuliishi na tulifanya shughuli zetu za kiuchumi na kijamii kwa kuheshimiana na kushirikiana bila ya kubaguana kwa ajili ya kutafuta fadhila na radhi za Mola wetu Mtukufu. Kwa hivyo, ni wajibu wetu tuiendeleze imani hio ya uchamungu tukijuwa kwamba, sisi ni wahitaji wa fadhila, baraka na neema zake katika kipindi chote cha maisha yetu hapa duniani na kesho akhera twendako.

Ni muhimu kwa kila mmoja wetu azingatie kwamba, utamaduni huu wa kuishi kwa kuvumiliana na kushirikiana tuliouonesha kwa kiwango cha

juu katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ni msingi muhimu wa kuilinda hali ya amani na utulivu ambayo Mola wetu Mtukufu ametujaalia nchini kwetu. Ukarimu, umoja na mshikamano wetu umekuwa ukipigiwa mfano katika nchi mbali mbali. Watu katika mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea wanavutiwa sana na hali ya nchi yetu na viongozi wa nchi hizo hawachelei kuelezea hisia zao za kuisifu Zanzibar namna tunavyoishi kwa amani, maelewano na udugu. Hii ni neema kubwa tunayopaswa kuifahamu na kuishukuru. Tuelewe kwamba bila ya kudumisha umoja na mshikamano wetu hatutaweza kupiga hatua za maendeleo.

### **Ndugu Wananchi,**

Natumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru masheikh, walimu na wanazuoni wetu, ambao katika maeneo mbali mbali walijitolea kuendesha darsa na kutupa mawaidha juu ya namna bora ya kuitekeleza ibada ya saumu katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ili tuweze kunufaika na fadhila zake. Wametukumbusha namna bora ya kufanya ibada mbali mbali na kuisisitiza juu ya suala la uchamungu katika mfumo mzima wa maisha kwa kipindi chote cha uhai wetu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu, Subhanahu Wa Taala, awalipe masheikh, wanazuoni na walimu hao kila la kheri na azikubali amali zao hizo kuwa ni "*Sadakatul Jariya*". Kadhalika, tunamuomba Mola wetu, nasi atupe wepesi wa nafsi katika kuyazingatia na kuyatekeleza yale yote waliyotufundisha kupitia mawaidha waliyokuwa wakiyatoa katika hadhara mbali mbali. Vile vile, nazipongeza Taasisi mbali mbali zilizokuwa zikitoa misaada kwa watoto yatima, wazee na wananchi

wengine, wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Hiyo ni ishara njema ya kutambua wajibu wa kusaidiana katika jamii yetu.

### **Ndugu Wananchi,**

Miongoni mwa mafunzo makubwa tuliyoyapata kwa kutekeleza ibada ya funga ni kuzielekeza nafsi zetu katika utii wa sheria za dini na sheria za nchi yetu. Kwa kila tulichokuwa tunataka kukifanya wakati tukiwa katika saumu, tulikipima kwa kuzingatia sheria. Tulizidisha nidhamu katika sehemu za kazi, tulizidisha stara katika mavazi, tulitumia maneno mazuri na kauli nzuri wakati wa mazungumzo yetu na tulizidisha heshima baina yetu. Inafurahisha kuona kwamba wananchi wengi walitii sheria na kanuni zinazotuongoza katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwani Uislamu unawataka watu wote waishi kwa kufanyiana mambo mema badala ya kufanyiana maovu kwa namna yoyote. Kwa hivyo, kama tulivyoweza kuishi kwa nidhamu na kutendeanana mema tukiwa na khofu ya kuudhiana, ili tusibatilishe saumu zetu; basi tuendeleo kuishi hivyo hivyo katika miezi mingine, ili tujiepushe na dhambi za kufanya maudhi ndani ya jamii. Katika kuonesha ubaya wa kufanyiana maudhi miongoni mwetu, Mola Wetu Muumba katika Suratul Ahzab aya ya 58 anatwambia:

***"Na wale wanaowaudhi wanaume waislamu na wanawake waislamu pasipo wao kufanya kosa lolote bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri".***

Kwa hivyo, ni vyema tuendeleo, kuyatekeleza majukumu yetu kwa faida ya kila mmoja wetu. Tujiepushe kufanya mambo ambayo yanawavunjia

heshima watu wengine katika jamii tunazoishi. Tukumbuke kwamba nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya sheria ambazo ni wajibu wetu sote tuzitii na tuzitekeleze. Sheria kuu ya nchi ni Katiba; ambapo ibara ya 11 (2) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984, inasema:

***"Kila mtu, anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake".***

Natoa pongezi kwa wananchi wote wa Zanzibar ambao si Waislamu, kwa kushirikiana na ndugu zao Waislamu katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kuishi kwa misingi ya kuheshimiana na kupendana. Ustahimilivu waliouonesha wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kielelezo cha kupevuka kwa ustaarabu wetu wa kustahamiliana pamoja na utamaduni mzuri tuliojijengea tangu kale na dahari wa kuishi pamoja bila ya kujali tafauti zetu. Hali hii imechangia sana kuiendeleza hali ya amani na utulivu tuliyonayo ambayo ndio msingi muhimu wa maendeleo. Tumuombe Mola wetu atujaalie tuwe wenye kufuata sheria katika shughuli zetu za kila siku na tuishi kwa kuzingatia maadili mema na aidumishe amani tuliyonayo nchini.

### **Ndugu Wananchi,**

Tunapaswa tuendeleo kutoa shukurani kwa Mola wetu Subhanahu Wa Taala kwa kuweza kuitekeleza ibada ya funga katika hali nzuri ya upatikanaji wa vyakula, kwani kadri tunavyozishukuru neema za Allah ndivyo anavyotuzidishia baraka. Katika Surat Ibrahim, aya ya 7, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

***... "Kama mkishukuru nitakuzidishieni; na kama mkikufuru, (jueni) kuwa adhabu yangu ni kali sana."***

Nafahamu kwamba bado kuna changamoto kwa baadhi ya familia zenye kipato cha chini ambazo hazikumudu kununua mahitaji yao ya vyakula kama ilivyotarajiwa, licha ya kuwepo neema ya upatikanaji wa vyakula mbali mbali katika maduka na masoko yetu. Tuiombe mema nchi yetu, ili Mwenyezi Mungu atupe mafanikio zaidi katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo yenye lengo la kuwanufaisha wananchi wote. Napenda nisisitize kwamba Serikali yetu, inafanya kila jitihada za kuuimarisha uchumi wetu, ili hatimae kila mwananchi awe na uwezo wa kukidhi mahitaji yake muhimu na kununua vitu anavyovipenda kwa ajili ya familia yake. Nnawashukuru na nnawapongeza wafanyabiashara wetu kwa kuhakikisha kuwa bidhaa muhimu ziliendelea kupatikana katika kipindi cha Ramadhani na hapana shaka zitaendelea kupatikana hata baada ya Ramadhani na hapo baadae.

### **Ndugu Wananchi,**

Katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kila mmoja wetu alionekana katika harakati za kufanyakazi, ili kukidhi ongezeko la mahitaji, hasa katika kutafuta sikukuu za watoto na familia kwa jumla. Sekta za kiuchumi, hasa biashara, kilimo, uvuvi, ufugaji na usafiri zilichangamkiwa na kuonesha taswira ya aina yake. Kwa hivyo, ni vyema tukahakikisha kwamba, katika miezi mingine, kila mmoja wetu anaiendeleza kasi na ari ile ile tuliyokuwa nayo katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa lengo lile lile la kuongeza uzalishaji na kipato kwa faida ya familia na nchi yetu kwa jumla.

Uislamu unatuhimiza kupenda kufanyakazi. Pale Muislamu anapofanya kazi kwa nia safi, moyo mkunjufu na furaha, anapata ujira kutoka kwa Allah Subhanahu wa Taala. Miongoni mwa sababu za kuumbwa kwa mchana ni kutuwezesha kufanyakazi vizuri. Mwenyezi Mungu ametuthibitishia jambo hili katika Suratu An Nabaa, aya ya 11 kwa kutwambia:

***"Na tukaufanya mchana kama kufufuka" (wa kuchumia maisha)***

Kazi ndiyo msingi wa kuchumia maisha. Historia inatueleza kuwa manabii nao walifanya kazi mbali mbali. Walikuwa wakijitafutia riziki kwa njia ya halali kutokana na nguvu zao. Mtume Daud (A.S) alikuwa fundi sanifu wa mavazi ya chuma kwa ajili ya watu kujihami vitani. Mtume Zakaria (A.S) alikuwa fundi seremala, Sayyidna Muhammad (S.A.W) alifanya kazi ya biashara na Manabii wengine wengi walifanya kazi ya uchungaji na nyenginezo.

Mtume wetu Muhammad (S.A.W), anatuhimiza Waislamu tupende kufanyakazi. Haya yanathibitika katika hadithi aliyoitoa na ikapokelewa na Abdillahi Bin Zubeir inayosema:

***"Mmoja wenu achukue kamba zake, kisha aende mlimani, aje na tita la kuni alilobeba mgongoni mwake na aliuze ni bora kwake".***

**Ndugu wananchi,**

Kwa hivyo, ni wajibu wetu kujenga utamaduni wa kupenda kufanyakazi. Hadithi hio, vile vile, inatuhimiza kuacha tabia ya kuchagua kazi, pale

ambapo kazi nyengine hazipo; hasa katika wakati huu ambapo tatizo la ajira ni changamoto kubwa hapa kwetu, katika nchi zinazoendelea na hata katika nchi zilizoendelea duniani. Jambo muhimu la kuzingatia hapa ni kufanya kazi za halali ambazo Mwenyezi Mungu anaziridhia.

Kwa bahati mbaya hivi sasa, wapo baadhi ya vijana ndani ya jamii yetu ambao wanachagua aina ya kazi za kufanya. Wanataka kazi za ofisini na kwenye vyombo vya ulinzi; ambazo ni chache hazitoshi. Wanapozikosa kazi hizo hupenda kuilaumu Serikali kwamba haiwapi ajira. Wajibu wa Serikali ni kuwapa elimu vijana wetu, ili waitumie katika kuyaendesha maisha yao. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwapa elimu vijana wake na wakati huo huo inaendelea kuandaa programu mbali mbali za kuongeza nafasi za ajira kwa kuzingatia utaratibu wa MKUZA III.

### **Ndugu Wananchi,**

Katika kuwasaidia wale ambao hawana ajira, hasa vijana, Serikali inaendelea kuuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi tuliouanzisha kwa kuuongezea fedha. Katika kipindi cha miezi kumi iliyopita; Julai 2017 hadi 30 Mei, 2018, jumla ya vikundi vya uzalishaji mali 90 vya Unguja na Pemba, vikiwemo vikundi 32 vya vijana na vikundi 9 vya watu wenye ulemavu vimepatiwa mikopo yenye thamani ya TZS milioni 695. Mikopo hio imeweza kutoa ajira kwa wananchi 2,013; kati yao wanaume 879 na wanawake 1134, katika sekta ya biashara, kilimo, ufugaji na viwanda vidogo vidogo.

Vile vile, Serikali inaendelea kushajiisha uundaji wa vikundi vya ushirika pamoja na kutoa mafunzo ya kazi na ujasiriamali kupitia vyo vya Amali tulivyovianzisha. Idadi ya vyama vya ushirika inazidi kuongezeka, ambapo hadi Machi, 2018 vilikuwa vimeshafikia, 3,333, ambapo Unguja vipo 2,198 na Pemba 1,135. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga jumla ya TZS bilioni 1.19 kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Nawahimiza vijana wafanye shime na hima ya kuzichangamkia fursa za uwezeshaji zinazotolewa na Serikali, ili waweze kujiajiri.

### **Ndugu Wananchi,**

Ili juhudi zetu za kupenda kufanya kazi ziwe na tija, ni muhimu tukazifanya kazi zetu kwa njia za kitaalamu na kwa uadilifu. Katika hotuba yangu niliyoitoa katika kilele cha Sherehe za Mei Mosi za mwaka huu, katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi - Wete Pemba, nilisisitiza haja ya wafanyakazi katika sekta ya umma na binafsi kufanyakazi kwa uadilifu na wasiwe wenye kutawaliwa na tamaa. Vile vile, nilisisitiza, umuhimu wa viongozi kuwa wabunifu na wenye kutumia vizuri elimu, ujuzi na maarifa, ili kuleta ufanisi katika sehemu zao za kazi.

Uislamu unatufundisha kwamba uadilifu na ujuzi ni vigezo muhimu ambavyo mwajiri anapaswa kuvizingatia kabla ya kuajiri, na sisi Serikalini tunavitumia vigezo hivyo. Tunajifunza katika maisha ya Nabii Mussa (A.S.) kwamba aliwahi kupendekezwa na watoto wa Nabii Shuaib aajiriwe na baba yao kwa sababu ya uadilifu aliokuwa nao. Haya

yanathibitika katika Suratul Qasas aya ya 26, pale Allah, Azza wa Jalla alipotuambia:

***Akasema mmoja wa wale wawili : "Ewe baba yangu! mkodi huyu. (awe anachunga wanyama wako badala yetu). Bila ya shaka mbora uwezaye kumwajiri ni ambaye mwenye nguvu, mwaminifu (Na huyu ana sifa zote hizo)".***

Kadhalika, Mola wetu Muweza anatufahamisha umuhimu wa kuwa na utaalamu au ujuzi wa kazi tunazozifanya au tulizoajiriwa kufanya. Maelezo ya Quran ya kisa cha Nabii Yusuf (A.S), katika Surat Yusuf, aya ya 55 yanatueleza:

***Akasema (Yusuf): "Nifanye mtazamaji wa hazina za nchi (yote); hakika mimi ni mlinzi mzuri na mjuzi hodari"***

Kwa hivyo, wafanyakazi wenzangu tulioko katika ajira ni wajibu wetu tuithamini na tuishukuru neema ya kupata ajira kwa kutekeleza dhamana na majukumu yetu kwa misingi ya uadilifu. Tuzilinde na tuziheshimu mali za umma na sehemu zetu za kazi. Tutambue kwamba kuna wenzetu hivi sasa wana mahitaji ya kutaka kufanya kazi, ili wawe wafanyakazi kama sisi, lakini bado hawajapata nafasi ya kuajiriwa. Tushikamane na tusiyumbe katika kuwa waadilifu kwenye kazi zetu. Tuendeleo kuvipiga vita vitendo vya rushwa na tuwafichue miongoni mwetu wanaofanya vitendo hivyo. Mafunzo tuliyoyapata katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ya kuwa wakweli, waadilifu, wenye kustahamili na kukinai nafsi zetu, tuyaendeleze mafunzo hayo na tuyatumie katika maisha yetu ya kawaida. Serikali kwa upande wake, itaendelea kuwachukulia hatua kali wale wote, wanaoendeleza vitendo vya rushwa,

wabadhirifu wa mali za umma na wanaoshindwa kusimamia dhamana walizopewa.

### **Ndugu Wananchi,**

Jamii yetu bado inakabiliwa na vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia. Ili tuweze kushinda vita vya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia, lazima kila mmoja wetu atimize wajibu wake kwa kuzingatia mpango wa miaka mitano (5) wa kupambana na unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia ambao tuliuzindua mwezi wa Agosti mwaka 2017. .Juhudi za pamoja zinahitajika katika kuutekeleza Mpango huu kwa ufanisi tunaoukusudia. Katika kuhakikisha utekelezaji wa mpango huo kwa mafanikio makubwa, naiagiza Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Wanawake na Watoto pamoja na kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kulishughulikia suala hili, waandae mafunzo maalum ya kuihamasisha na kuielimisha jamii na sekta zinazohusika, ili waufahamu wajibu wao katika kulimaliza tatizo hili. Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama zetu, nazo ziendeele kuyatekeleza majukumu yao vizuri, ili kesi za udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia ziweze kusikilizwa kwa haraka. Kadhalika, Viongozi wa Mkoa na Wilaya itawalazimu waandae kazi zenye kutoa matokeo ya haraka zaidi katika kuendesha mapambano haya. Ni muhimu kwa kila Mkoa kuweka takwimu sahihi za vitendo hivyo, ili zisaidie katika kufanya tathmini na kuandaa mikakati imara.

Miongoni mwa jitihada za kuhakikisha kwamba tunatimiza wajibu wetu katika kuzingatia mpango wa miaka mitano (5) wa kupambana na unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia; wazazi na walezi sote inatulazimu tuongeze nguvu na tushirikiane katika malezi ya watoto wetu. Ni lazima, tuifuatilie mienendo ya watoto wetu. Vile vile, tuisite kuwahoji pale ambapo tunawaona na vitu ambavyo hatuelewi wanakovipata. Tujifunze kwa Nabii Zakaria (A.S), mlezi wa Bibi Maryam binti Imran. Katika Surat Al Imran, aya ya 37, Quran inatupa mafunzo hayo kwa kusema:

***“... Kila mara Zakaria alipoingia chumbani (kwake Maryam) alikuta vyakula pamoja nae (huyo Maryam). Akasema, Ewe Maryam unapata wapi hivi?”***

Hivyo, na sisi tuwalize watoto wetu, umevipata wapi hivi maana dunia imeharibika.

### **Ndugu Wananchi,**

Kwa mara nyengine, napenda kuwaasa wazazi na walezi kwamba, inapotokezea kosa la udhalilishaji ambalo limefanywa na mtu wa familia, hatupaswi kabisa kulitolea hukumu na kulimaliza kifamilia. Tunapoamua kuyamaliza matatizo haya kifamilia au kuchelea kutoa ushahidi sahihi katika vyombo vya sheria, inakuwa ni sawa na kudhoofisha jitihada za Serikali na kuyaendeleza maovu.

Mwenyezi Mungu anawambia katika surat Al Anaam, kwenye sehemu ya aya 152:

***"... Na msemapo (katika shahada na penginepo) semeni kwa insafu ingawa ni jamaa,(usimpendelee kwa ajili ya ujamaa uliyo baina yenu)".***

Naamini kwamba umoja ni nguvu, na iwapo kila mmoja wetu atatekeleza ipasavyo wajibu wake katika mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na udhalishaji wa watoto, Inshaallah, tutafanikiwa.

### **Ndugu Wananchi,**

Kujaaliwa kupata watoto ni jambo jema kwa familia na taifa kwa jumla. Katika Quran Tukufu jambo la kupata mtoto, limetajwa kuwa ni ishara njema. Tukirejea katika Surat Maryam aya ya 7, Mwenyezi Mungu anamwambia Nabii Zakaria:

***"Ewe Zakaria! Tunakupa habari njema ya (kuwa utazaa) mtoto, jina lake ni Yahya....."***

Kwa hivyo, ni wajibu wetu kushukuru neema ya kupata watoto kwa kuwapa malezi na kuwaepusha na vitendo viovu, vikiwemo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji ni wajibu wetu, vile vile, tuzingatie suala la kuendeleza malezi bora ya watoto wetu kwa mujibu wa maadili, silka na utamaduni tulioachiwa na wazee wetu. Nyote ni mashahidi kuwa malezi yetu hivi sasa yana mtihani mkubwa. Kila mzazi na wanawe. Hapo zamani watoto hulelewa na kiambo au mtaa mzima. Kila mzee katika mtaa alikuwa ni mzee wa watoto wote na walitakiwa

wamuheshimu na wamtii. Utamaduni huu ulisaidia sana watu kuheshimiana na kuwapa usalama watoto katika mitaa, hata pale wazazi wao wanapokuwa hawapo.

Katika juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuzilinda mila zetu, silka zetu na utamaduni wetu, Serikali imeunda Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale pamoja na Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara hizi, pamoja na mambo mengine, zimeundwa, ili kuhakikisha kwamba mambo yetu ya asili yanadumishwa, silka zetu na utamaduni wetu unaendelezwa. Miongoni mwa mambo ya utamaduni yanayopaswa kusimamiwa kwa karibu ni silka na malezi ya watoto wetu. Kwa hivyo, wazazi na walimu tuna wajibu wa kushirikiana katika kuhakikisha kwamba jamii yetu inapata mustakabali mwema.

### **Ndugu Wananchi,**

Malezi bora ndio msingi wa kupata raia wema, wazalendo na watakaotuwezesha kuwa na jamii yenye maadili mema. Miongoni mwa jitihada za kuwajengea watoto wetu misingi imara ya maisha yao ya baadae, ni kuimarisha ustawi wao na kuwaandaa kuwa raia wema wenye elimu, maarifa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya karne ya 21. Katika kuyatekeleza mambo hayo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imefanya juhudi kubwa katika kuimarisha sekta ya elimu, kuanzia elimu ya Maandalizi, Msingi, Sekondari hadi Chuo Kikuu. Mwaka 2016/2017 Serikali iliondoa michango ya wazazi kwa skuli za msingi na mwaka wa fedha 2018/2019 imeondoa michango ya wazazi katika kugharamia elimu ya Sekondari na sasa itatolewa bila ya malipo. Kwa hivyo, elimu ya Msingi na Sekondari sasa itatolewa bure hapa Zanzibar.

Hatua hio, ina lengo la kutekeleza dhamira ya Mapinduzi yetu Matukufu ya 1964, kwa misingi ile ile iliyoasisiwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ya kutoa elimu bure kwa watoto wote wa Zanzibar bila ya ubaguzi.

Katika kuona kuwa watoto wetu, hasa wa Skuli za Sekondari wanapata mazingira mazuri ya kusomea, Serikali imeiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilifanyie kazi suala la kuziendeleza huduma za dakhalia kwa ukamilifu. Serikali itahakikisha kwamba huduma za dakhalia zinaendelezwa na zinafanikiwa. Huduma hizi, mbali ya kuwapa wanafunzi muda mzuri na utulivu wa kushughulikia masomo yao, vile vile, wazazi wanapata utulivu kwa kujua kwamba watoto wao wanaishi katika mazingira yaliyo salama. Kadhalika, maisha ya dakhalia huwasaidia watoto kujuana na kujenga nidhamu ya uzalendo, ambalo ni jambo la msingi katika kujenga umoja wa kitaifa. Vile vile, dakhalia zinawafunza watoto mbinu mbali mbali za kukabiliana na maisha wakati watakapoishi mbali na familia zao.

### **Ndugu Wananchi,**

Kuwepo kwa tatizo la mmong'onyoko wa maadili katika jamii yetu kunachangiwa sana na athari za malezi na uvunjaji wa sheria. Hivi sasa, tunasikia malalamiko kutoka hospitali zetu kwamba baadhi ya watoaji huduma za afya hutumia lugha isiyofaa kwa wagonjwa. Baadhi yao wanakwenda kinyume na maadili ya kazi zao na wengine hawazingatii sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake. Inatupasa tuelewe kwamba maadili mema yanatuepusha na migongano katika jamii. Vile vile, huwaepusha vijana wetu na vitendo vinavyoweza

kuathiri maisha yao, ikiwa ni pamoja na matumizi ya dawa za kulevya na matumizi mabaya ya mitandao. Vile vile, maadili mema yanaiongoza jamii katika kuzingatia umuhimu wa kuyalinda mazingira na kudumisha usafi, kuishi vyema kwa salama na kupata ustawi katika jamii yetu.

### **Ndugu Wananchi,**

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa salama bila ya kukabiliwa na miripuko ya maradhi, hasa kipindupindu. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, miripuko hii ya maradhi ilikuwa ikiathiri baadhi ya tamaduni zetu, kama vile kula pamoja katika mikusanyiko. Hata hivyo, hatuna budi tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake, kwa mwaka huu kutujaalia mazingira mazuri yaliyopelekea kuifunga Ramadhani kwa salama na amani.

Vile vile, natoa shukurani na pongezi kwa wananchi kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya katika kukabiliana na kujikinga na maradhi ya miripuko na kudumisha usafi. Ni wajibu wetu tuendeleze kwa furaha mwenendo huo, ili tuweze kuishi kwa salama tukiwa na siha njema.

Serikali inaendelea kuchukua hatua, ili afya za wananchi ziendeleze kuimarika kwa kutekeleza mikakati mbali mbali, ikiwemo kuongeza bajeti ya Sekta ya Afya pamoja na bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa vya utibabu. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga jumla ya TZS bilioni 12.7 kutoka TZS bilioni 7.0 za mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 81.4, kwa ajili ya ununuzi wa dawa na

vifaa vya utibabu. Kadhalika, Bajeti Kuu ya Wizara hio, imeongezwa kutoka TZS bilioni 72.9 mwaka 2017/2018 hadi TZS bilioni 93.2 mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 27.8 na kwa hivyo huduma za afya zitaimarishwa katika Idara zote kama hotuba ya Waziri wa Afya ya Bajeti ya mwaka huu ilivyofafanua.

Bajeti hio itaiwezesha Serikali kuendeleza lengo la Mapinduzi Matukufu ya 1964 la kutoa huduma za afya bure kwa msingi wa usawa kwa wananchi wote wa mjini na mashamba, kwa Unguja na Pemba.

### **Ndugu Wananchi,**

Leo ni siku ya furaha kwa Waislamu wote duniani, wananchi wote wa Zanzibar walio Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Isitoshe, ni furaha kubwa kwa familia zetu hasa watoto. Ni siku ambayo familia zetu hupata wasaa wa kukutana na kutembeleana kwa furaha. Kwa hivyo, nasisitiza juu ya kuisherehekea vyema sikukuu yetu kwa kufanya mambo ya kheri yakiwemo kula na kuvaa vizuri, kuwatembelea wagonjwa, jamaa, ndugu na marafiki.

Nawatakia matayarisho mema Waislamu wote wanaojiandaa kwenda kuitekeleza ibada ya Hijja mwaka huu. Naamini mtashirikiana vyema na watendaji wetu wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Taasisi nyengine, ili safari yenu hio iwe nyepesi na ya kheri, msipate usumbufu wowote, kabla ya safari, wakati wa Hijja na mnaporejea nyumbani.

Napenda niwafikishie mahujaji na wananchi wote wa Zanzibar, salamu za pongezi kutoka kwa Sheikh Saleh bin Abdul Aziz bin Muhammad; Waziri wa Saudi Arabia aliyekuwa anashughulikia Mambo ya Kiislamu,

Da'wah, Misaada, Mafunzo na Miongozo. Sheikh Saleh alinipa salamu hizo takriban wiki mbili zilizopita, hapo tarehe 30 Mei, mwaka huu aliponitembelea ofisini kwangu Ikulu. Alitupongeza kwa tabia njema, ukarimu na upole unaooneshwa na mahujaji wa Zanzibar wanapokuwa katika mji Mtukufu wa Makka kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Hijja au Umra. Hii ni sifa njema tunayopaswa kuiendeleza kwa umoja wetu na kwa nguvu zetu zote. Vile vile, katika mazungumzo hayo, nilisisitiza haja ya kuimarisha ushirikiano na ndugu zetu wa Saudi Arabia kwa kuwashauri wafungue ofisi ndogo ya Ubalazi hapa Zanzibar, hatua ambayo itaimarisha uhusiano wetu na kupunguza usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa matayarisho ya kwenda Makka kuhiji.

### **Ndugu Wananchi,**

Pongezi na shukurani maalum nazitoa kwa wale wafanyabiashara walioitikia wito wa Serikali wa kutopandisha bei za bidhaa za chakula baada ya Serikali kuwapunguzia ushuru. Kwa uamuzi wao huo, hawakupata hasara na wala hawakupoteza chochote, isipokuwa walijiongezea baraka katika biashara zao. Kadhalika, natoa pongezi kwa wakulima wote kwa juhudi zao walizozichukua kwa kuhakikisha kwamba mazao mbali mbali ya matunda na vyakula maarufu yalipatikana kwa ajili ya futari. Tumuombe Mwenyezi Mungu atuongezee neema hio.

### **Ndugu Wananchi,**

Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ulikutana na vikao vinavyoendelea vya Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, natumia fursa hii, kumpongeza Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kviendesha vizuri vikao vya Baraza vya Bajeti kwa mafanikio makubwa.

Kadhalika, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kwa kuzijadili Bajeti za Wizara za Serikali, kutoa maoni yao na mapendekezo na hatimae kuzipitisha Bajeti hizo. Wananchi wanafuatilia na wanafarijika kutokana na juhudi zenu za kuzitafutia ufumbuzi kero na changamoto mbali mbali zinazowakabili katika maeneo yao.

Naupongeza Uongozi wa Baraza la Wawakilishi, Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale na Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kwa kuendelea na utaratibu wa kuonesha moja kwa moja vipindi vinavyoendelea katika Baraza la Wawakilishi, jambo ambalo linawasaidia wananchi kuyafahamu masuala ya msingi yanayowasilishwa na Wawakilishi wao. Kadhalika, vipindi hivi huwawezesha wananchi kupata majibu ya moja kwa moja ya kero zinazowakabili kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri. Natoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri kwa umakini wao katika kujibu hoja na maswali mbali mbali kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nawahakikishia kuwa Serikali inaheshimu michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na tutaendelea kuifanyia kazi kwa lengo la kuzidi kupiga hatua za maendeleo nchini kwetu. Kwa niaba ya Wananchi wote nakutakieni kila la kheri, ili mmalize vikao vilivyobakia kwa mafanikio makubwa zaidi.

### **Ndugu Wananchi,**

Nikiendelea kutoa pongezi na shukrani, napenda niwashukuru na niwapongeze viongozi na wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa kazi nzuri waliyoifanya ya utekelezaji wa maagizo

niliyoyatoa ya kuwapelekea maji wananchi waliokuwa na matatizo ya kukosa maji katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Jitihada zao walizozifanya zilisaidia sana katika kuwaondolea wananchi usumbufu wa kutafuta maji. Vile vile, shukurani zangu ziende kwa Jeshi la Polisi, hasa askari wa usalama barabarani, kwa kusimamia sheria na kudhibiti ajali zisizo za lazima. Hata hivyo, wanapaswa waongeze juhudi zao katika kipindi hiki cha sikukuu na baada ya sikukuu, kwa kuhakikisha kwamba kunakuwa na askari kila wakati katika maeneo ambayo yamekuwa na msongamano mkubwa wa magari.

Kama tunavyoelewa kuwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ulikutana na kipindi cha mvua kubwa za masika ambazo kwa baadhi ya maeneo zimesababisha maafa kwa wananchi na vitu vyao. Ntoa mkono wa pole kwa wale wote waliofikwa na maafa na kuwaombea Mola awape subira.

### **Ndugu Wananchi,**

Namalizia hotuba yangu kwa kukutakieni wananchi nyote amani na furaha katika kusherehekea sikukuu hii ya Idd el Fitr. Mwenyezi Mungu atupe uhai na uwezo na atujaalie tuweze kuzifunga Ramadhani zinazokuja na tunufaike na fadhila zake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie amani, umoja, utulivu na mapenzi baina yetu. Atupe mvua zenye baraka ya mazao na atuepushe na majanga. Awape afueni wagonjwa wetu walioko majumbani na kwenye hospitali zetu. Awasamehe makosa yao, ndugu, jamaa na wazee wetu wote waliokwisha tangulia mbele ya haki. Atupe khatima njema na sisi tulio

hai. Mola wetu atujaalie tuisherehekee sikukuu hii na nyengine zijazo kwa amani na turudi nyumbani kwa salama.

**IDD MUBARAK**

**KULLU AAM WA ANTUM BIKHEIR**